TANGAZO LA SERIKALI NA. 641 la tarehe 26/7/2024

SHERIA YA OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA,
(SURA YA 430)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1))*

NOTISI YA UTEUZI WA WAENDESHA MASHTAKA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uteuzi wa Waendesha Mashtaka ya Mwaka 2024.

Uteuzi wa waendesha mashtaka

2. Watu ambao majina yao yameorodheshwa katika Jedwali wameteuliwa kuwa waendesha mashtaka kwa madhumuni ya kuendesha mashauri ya jinai kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Uhalali wa uteuzi

3.-(1) Mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya Notisi hii atatumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Notisi hii.

(2) Bila kujali ujumla wa aya ndogo ya (1), mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya Notisi hii anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kinachopungua miaka mitano endapo ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma itakoma au uteuzi wake utatenguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| S/N | JINA |
|---|---|
| 1 | Isaack Athanas Nyimbi |
| 2 | Amina Greyson Mziray |

*Tangazo La Serikali Na. 641 (Linaendelea)*

| | |
|---|---|
| 3 | Nicodemus Sospeter Kusenha |
| 4 | Prosper Romanus Malangalila |
| 5 | Victorino Ladislaus Kuluchumila |

Dodoma
7 Juni, 2024

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU
*Mkurugenzi wa Mashtaka*